(inaudible) basi anaweza kusema sasa anamua mtu ili hawa watu wetu ambaye wako na mali wapate kuchukuliwa fine. Sasa ninaona ni vyema mtu akimua mtu, sheria ifanye (inaudible) na mtu kama huyo apate kuadhibiwa kama ni kufungwa na watu wa wache wakae vile walikuwa hapo mbeleni. Kwa sababu haiwezekani isemekane kwamba mtu wetu fulani amue mtu tuseme hapa West Pokot, halafu utaona watu wanakuja kwangu ati wanataka ng'ombe ati kwa sababu ndugu yangu amemua mtu. So ninaona jambo hilo ni kama kinyama kabisa, na njia wananyanyasa watu bure.

Jambo ingine basi ningependa kusema ni kuhusu hii wizi wa mifugo ambaye imeendelea mara mingi kwa sehemu hii. Tumeona sana kwamba Serikali wanaona tuseme kama Pokot na Turkana wameuana hapa na badala yakutafuta dawa yakumaliza hiyo jambo, hawashughuliki jambo hilo kabisa. So ningesema kama tuseme kama kuna kabila ambaye inauana heri ifanywe kuweka hapa kambi ya Jeshi, halafu itakuwa ikipunguza kuzuia jambo kama hilo ambaye inatokea mara kwa mara.

Jambo lingine ambao ni la mwisho jambo ambaye sasa inaendelea sana sehemu hii tumeona kama sehemu zote boma kuna wanaume ambaye wamekuwa wakubwa, kuna hata wengine kunaye wana uwezo ambapo kama mzee fulani akikuja utakuta msichana ambaye ni wa mwaka kumi na nane anaanza kwa mzee wa mwaka sabini na wale wandugu zake wakijaribu kutakaa, yule msichana anapeanwa na anapeanwa utakuta msichana fulani anaenda kufika kwa ile boma ya mzee kwa ababu hataki anaenda kukunywa dawa ama ku-commit suicide na anakufa kwa jambo kama hilo. So ningetaka kwa sheria ya sasa ipate kutetea haki ya kila mtu. Msichana akisema sitaolewa na mtu fulani hiyo pia ipate kuangaliliwa na kuwe na sheria ambayo ni serious. Asanteni.

**Leiro:** Asante sana Bw. Julius Torong, umetumia wakati mzuri, mwenye atakuwa anafuata sasa ambaye atapeana maoni yake kwa mbele ya Commissioners, Akilora hayuko, na kama hayuko Apeyok Loteko, Karibu

**Loteko Apeyok:** Jina langu ni Loteko Apeyok.

**Loteko Apeyok:** Kainenyaan kuu Loteko Apeyook,

**Translator:** Kwa upande huu wetu.

**Loteko Apeyok:** Ompo koroo neete,

**Translator:** Hapa Tangulbei.

**Loteko Apeyok:** Yetee lee Tangulbei,

**Translator:** Ningependekeza hivi.

**Loteko Apeyok:** Ko-omwoghan loo,

**Translator:** Katiba hii itupatie watu wa Tangulbei hospitali yetu.

**Loteko Apeyok:** Mchiini katibanu po yee ku-koneecha skutali nyoo

**Translator:** Na pia Serikali ijengee D.O. nyumba na Ofisi hapa Tangulbei.

**Loteko Apeyok:** Mchiini kteekchuu Soch koo D.O. nko ofis yetee lee Tangulbei

**Translator:** Tena.

**Loteko Apeyok:** Napooh,

**Translator:** Jambo ambaye pia Katiba hii izingatie.

**Loteko Apeyok:** Kiito anga nyo mchiini kuroos katiba nuu,

**Translator:** Nataka Tangulbei iweke maji, watu waone maji.

**Loteko Apeyok:** Omochan Tangulbei kutoo pogh kusuuk piich pogh tukuul.

**Translator:** Dam kubwa.

**Loteko Apeyok:** Lenyee otupoo pogh nyo kikipaal nyo wou.

**Translator:** Nataka mahali inaitwa Ayam iwekwe Dam kubwa

**Loteko Apeyok:** Omochan owaan.

**Translator:** Asante sana mzee hayo tu ni yangu.

**Leiro:** Mwingine ambaye anafuata ni John Lobureria

**John Lobureria:** Majina kamili ni John Lobureria. Kwa siku ya leo nina machache, ni machache kwa Katiba ya wakati huu vile nimeonelea ingekuwa kuliko vile ilivyokuwa. Kuna mambo machache hapa, mara kwa mara kama watu wengi wameongea, lakini kwa upande wangu kwa upande wa afya, nitapenda hivi, kama community hii yetu tuna shida kubwa kwa upande wa matibabu tuseme hata hivo, hospitali ikifika ile gharama mtu akipewa, tuseme amepolekwa hospitali kuna ile calamity mtu anaweza kushtakiwa na ulemavu fulani ama amepata shida fulani kubwa kwa sehemu ile ya sensitive kama ya figo, roho wapi, ku-meet hiyo matibabu ni vigumu, kwa hivyo Katiba hii kama Pokot at least wazingatiwe kwamba watu kama hawa wameangaliliwa iwe ni special case hata NGO fulani iwe applied ili ishughulikie tatizo kama hilo.

Ingingine ile ninaonelea zaidi ni ile boundary changes watu wameongea lakini sija tosheka kusema. Asili yetu nafikiri tukikumbuka ama tukirudi 1910 vile watu walivyo sema kuna ile inaitwa Suk boundary, hiyo boundary iwe drawn properly sababu mali asili inategemea wale wameepuka kwa hivyo kurudia mpaka boundary kama hiyo mpaka tupate, tunajua ni shida na ni vigumu na tukasahau tunaongea lakini hatuta saha. Yule atazaliwa hata watoto wale wanazaliwa watakumbuka kwamba ardhi yao imepokonywa kwa njia isiyo halali.

Pia upande ya mwanadamu, ukikuta mtu anakutwa na wildlife, ile maiti ya huyo mnyama itakuwa ni kubwa kuliko maiti ya mtu. Utakuta mtu amelipuliwa na risasi maisha amepoteza hakuna atakaye shughulikia, sijui ni kwa sababu watu wetu hawajui vile yakushughulikia maneno kama hiyo ama ni nini. Kwa hivyo kwa upande huo lazima tuangaliliwe.

Kwa hivyo kwa upande wa elimu, elimu lazima iangaliliwe vizuri kwamba Chief's Act kutoa watoto vile watu wamesema, itolewe na kundi lakusomesha watoto liwe ni lakuzingatiwa kwa njia inayo faa. Siyo ati watoto wateswe tu kisha wanawekwa. At least tukisema, tunatarajia mazuri ama tuseme progress. Asante.

**Leiro:** Asante sana Bw. Lobureria. Mwenye tutakuwa naye sasa ni Pastor Joseph Akai

**Pastor Joseph Akai:** Nashukuru sababu ya nafasi nzuri kama hii. Maoni yangu naonea kuhusu mambo ya .....community yetu ya Pokot imekuwa na shida nyingi sana kwa mambo ya mipaka na tumepoteza ardhi zetu kuhusu mambo ya mipaka. Sehemu nyingi kama Lorien, ama sehemu kama (inaudible) naona ya kwamba zamani kidogo ilikuwa na sehemu zetu lakini kufikia wakati huu sio yetu na tukaona ya kwamba ingekuwa vizuri Serikali kuwatilia maanani kuangalia kilicho fanyika mpaka mipaka ikaonekana ya kwamba ilitoka ingeenda hatua ya mbele na ikarudi hatua karibu ya tatu, na nini ilifanyika.

Ya pili tena, ningeeonea kuhusu mambo ya wanyama. Tumepoteza kitu kiwili kwa sababu ya wanyama. Na tungeona ya kwamba heri Serikali wangeona watatufanyia wangetufaa tu kuhusu hali ya wanyama wa pori. Kwanza ukilima shamba yako na wakati unalima, ndovu zikakuja na zika kula mimea zako, wakati zinapo..Serikali imesema ya kwamba haitakikani kabisa mtu kuguza wale wanyama. Wewe sasa hata ukipiga nduru ufanye nini, watakukimbia watafukuza watuagamiza. Utapoteza chakula, utampoteza mtu na tunaambiwa ya kwamba tunahitaji kila mtu, tunahitaji tuagamize njaa. Tutaangamizaje njaa, kama wanyama wanatumaliza pamoja na chakula? Tutawezaje kuagamiza njaa? Kwa hivyo hapo Serikali wangechukua hatua kabisa waone ya kwamba watafanya nini ili wapate kuokoa vitu kama hivyo sababu raia zaidi upande ya taifa. Lakini kama raia wanaumia na kuagamia na uongozi unaonekana ya kwamba itakuwa ni nzuri, itakuaje nzuri kama raia wanaumia? Raia tukimalizika mtaongoza nini? Kwa hivyo ingekuwa ni vyema muaangalie vizuri sana kwa Katiba ya sasa.

Nyingine tena kuna kitu ambaye inatuletea hasara kabisa, haswa sisi kama raia wa sehemu kama hapa, tumewapoteza watoto wengi sana kwa sababu ya wengine kuwadunga mimba na kukataa, jinsi wa mama walisema saa zile. Hiyo kitu imeenea sana siku hizi. Na tungesema ya kwamba Serikali watilie maanani, vile wa mama walisema ni hiyo ni kitu ya kweli kabisa, kama itakuwa ni ngombe kumi na tano, iwe ni ngombe kumi na tano, kama vile wa mama wamesema ni ngombe kumi na tano mbuzi thelathini iwe ni hivyo kabisa. Kwa hivyo sitaendela na Mungu awabariki.

**Leiro:** Asante sana Pastor, umejaribu sana kufupisha, mwenye nitakuwa naye ni mtu wa mwisho kulingana na ile orodha ilipeanwa hapa ni Daniel Kapedo, Daniel Kapedo kuja upeane maoni yako hapa mbele ya hawa Commissioners.

**Daniel Kapedo:** Asante sana kwa nafasi ambaye nimepata, tunakuja kuchelewa na majina ni hayo yaliyosemwa Daniel Kapedo, nina maoni sijui kama wenzangu wamepitia ama hawajapitia, ya kwanza ni kura katika nchi Kenya inatakiwa kuwa ya siri, hii mambo ya mlolongo baadaye mwingine ataweza kuumizwa kwa sababu alikuona una—ule mwingine, kama ni KANU ama chama gani hatutaki mambo yakudanganyana ati watu waende kwa mlolongo kama mbuzi. Wanatakiwa kupiga kura ya siri ambaye siri haijulikani ulimpigia nani kura.

Jambo la pili ni pay ya wajumbe ambaye wanapeleka kwa hii bunge, sijui kama watapitisha, na wakipitisha watakuwa

wamefanyia Kenya unyama na inaonekana ati wanawakilisha Kenya. Mtu moja alipwe 3.6 million na wengine wana lala njaa vibaya, kwa hivyo tunapinga hoja hiyo ya bunge, wabunge kujilipia pesa nyingi. Kama kila mtu ana decide pesa ambaye atalipwa na anapitisha, natuelewe tuko katika third world country kwa hivyo kila mtu aki..yaani mtu moja alipwe 3.5 million, kwa hivyo maoni yangu nikupinga hoja ambaye wabunge wanapeleka bunge yakusema ati walipe mtu moja 3.6 million hiyo ni mbaya. Hiyo pesa ingefaa kukopeshea watu wengine.

Jambo la pili ambayo inafuatana na ya wabunge, uwakilishi mzuri hauko katika Kenya kwa sababu gani, katika hizi area ambaye ni za nomads, some areas are very big hata nyinyi ambaye mko sehemu hii mtaenda Kollowa, mtaenda Nginya, so Kollowa is about 180 kilometers at the end of this Baringo constituency na hauja fika mwisho hapa na inasemekana ni mtu moja, ikiwa ni mbali musiseme ati ni idadi, (inaudible) Lodwar district, na wenye waliunda Katiba ya kwamba walisema nchi hii mtu (inaudible) 40,000 people lakini ingestahili kuangaliwa kwa makini geographia ya zile nchi badala ya mtu moja kuwakilisha dunia mzima.

Ya tatu kufuatana na hayo, kuna msemaji moja alisema wakati niliingia ya kwamba Councillor wamefanyiwa dhambi, ingefaa walipwe na Central Government kwa sababu district ingine katika Kenya haina uwezo wakulipa ma-councillors. Ukienda sehemu kama (inaudible) watu wana wildlife nyingi, watu wana tourist kwa wingi unaweza kuona Councillor anaweza kulipwa 70,000/ ni si shida lakini ukikuja sehemu kama Baringo uende hata Mandera ama Wajir hakuna resources yakulipa Councillor anaenda 5 years bila kulipwa mshahara, wananchi wanataka watumikiwe na Councillors kwa hivyo MP can pay the Councillors kwa sababu wote wanawakilisha hawa wananchi pamoja kwa hivyo Councillors wangelipwa katika Central Government.

Jambo lingine sisi sijui kama tunaitwa kama Pokot ama nini ama nomads, ukikuja kufika Lorup unakuta mwisho wa lami halafu utatembea murrum, sijui dust na nini kwa Tambach, kama nyinyi Commissioners mtakuwa hapa, sijui kwa sababu hatuwakilishwi sijui Serikali yetu inakuwa mbaya kwa watu wengine, kwa hivyo kuna mtu alisema marginalized, kweli tumekuwa marginalized kuna watu wamesoma hakuna moja ana cheo yeyote katika Serikali. Mwisho sijui ni D.O. ama nani. Kwa hivyo ingekuwa ni jinsi Councillor moja amesema ati, 'oh we should a district atleast'.

Kwa hivyo mungepata resources yetu kama Serikali katika central government inatuma ya maendeleo ikagawanywa wale ambao wako katika hiyo district, saa hii (inaudible) hata hawapatikani. Unaweza kuta Mwalimu moja anafunza one to four shule moja, ako shule moja, lakini ukienda ...ya Baringo watu wote wanasanyana huko hakuna mtu anafundisha lowlands huko, it is forgotten, kwa hivyo tungekuwa na district hiyo share ya district watu wetu wangeajiriwa sawa sawa na watu wetu tungeangalia hata watu wetu ni shule gani haijapata na kuweka staff. Lakini kama ni huko district, Kabarnet ndiyo wanatutumania upande huu, mpaka Kollowa mwisho dunia ile ni shida. Kama kuna district nyingine katika this (inaudible) land ambaye iko shida kama ile tunaye wanaumia.

Kwa hivyo hatutaki watu wengine wafaidike katika taifa ambaye sisi ni wana Kenya na wengine wafaidike. Kwa hivyo ni heri

kila mtu katika Katiba wapewe afadhali (inaudible) Lancaster house na Constitution Review ama ripoti, tunaomba Commissioners musifiche ya wale ambaye marginalised na wale ambaye wanaogopa sijui nini, kwa hivyo maoni ya kila mtu lazima iwekwe vile imetoka ndiyo watu wajue kuna shida.

Jambo lingine ni freedom of worship. Hii uhuru wakuabudu, kuna dini nyingi ambaye imekuwa registered katika Kenya ambaye unakuta una register hata dini ya kishetani halafu unsema Commissioners to look into devil worshippers. Katiba inge control hiyo freedom imekuwa misused, imeharibiwa kwa sababu hata isemekane hata form kanisa katika jina amri ya kanisa lakini ni shetani. Kwa hivyo hii uhuru yakuabudu lazima Katiba ya sasa ituhakikishie sisi hiyo uhuru yakuabudu isitumike vibaya.

Jambo lingine ni political parties. Sijui kama itakuwa controlled ama haitakuwa controlled lakini maoni yangu it has become too much, but (inaudible) hii imetokea mtu akifilisika anaunda chama anaenda saa nyingine foreign countries kuomba donors at kwa chama ya kuku ama chama ya nini na kumbe anataka kujitajirisha kwa hivyo chama hii ambaye ni (inaudible) uhuru ya kuunda chama at least lazima iwe (inaudible) hii chama imekuwa nyingi na watu sasa wanaenda wanafaidika bure kwa kupitia jina yakusema chama.

La mwisho, kuna mtu aliongea mambo ya magari nzuri nzuri, Katiba ya good governance haitaki gari, unakuta location inaweza ku-allocate kama vile tunapatiwa, yaani anapatiwa vote ya hiyo Ministry lakini ukirudi mpaka grassroot huko chini unakuta chief officers ambaye hawana manyumba , hawana magari, Polisi wana lala ndani ya nyumba ya watu watano, kwa hivyo Serikali ni sharti wajenge manyumba ya civil servants ama staff, how serious utaenda kutana mwanaume na mwanamke mwingine wanashare nyumba na huyu mtu ana bibi yake. Bibi yake anaweza (inaudible) kwa hivyo ninaomba Katiba iangalie ya kwamba (inaudible) structures kama Police station watu hapana omba, hakuna haja yakujenga Police Station yaani one office two houses for twenty people, hiyo ni unyama hairuhusiwi maana huyu mtu anatakiwa kuishi na kulala ni private kwa hivyo Serikali hapa waweke structures katika sehemu ambayo tangu kuanzisha vitu, ama kama ni headquarters ya D.O. ana headquarters ya Police ama lazima waweke structures.

Yamwisho ni mamba ya tohara, ati msichana atahiriwe ni mbaya kwa sababu gani ukimwi. We we in Pokot bado hujui mambo iliyo wapata watu na ukimwi ndiyo unatahiri msichana, kama hujui ukimwi inaua, itaua mtoto wako wewe bila kupenda, hata akifanya ile mambo, lakini akitahiriwa anaweza kushikwa kwa sababu wakiwa wanne, na moja awe na ukimwi wote watakuwa infected. Tunaendelea watu wana erevuka kwa hivyo mambo yakutahiri ikishwe hakuna haja. Ya mwisho ni maoni hii mambo ya Lapai mtu akiua mtu, (inaudible) kama hakuna polisi karibu hiyo .....security katika nchi za kavu kama hapa, so ukifika hapa (inaudible) kwa sababu mtu akimuua mtu hapa tuseme ati uende utafute Police Kabarnet wakati ambae Police watakuja huyo mtu yuko Nairobi. Nani atamuongonjea huyo mtu atakuwa amepotea kwa hivyo kama ningekuwa , kama ni mimi kwa maoni, hiyo kitu kidogo ingekuwa hawa watu mpaka ingekuwe Serikali karibu security vile watu wanaongea mambo ya security police wakuje karibu, kuna 999 kuna nini, ambaye ikishout ya switch a button kuna gari ya police inaingia, lakini kama ni kwenda mguu mpaka Kabarnet, unatafuta Police unatafuta mtu amemuua mtu, afadhali huyu mtu akilipishwa fine ataogopa watu wako

na ng'ombe mingi hapa. Yangu ni hayo asante.

**Leiro:** Asante sana, unaweza pita upande ule upeane jina lako. Kuna mtu moja ameomba kwamba kuna jambo la maana sana ambaye hakuna mtu amezunguza juu yake tutampatia huyu Samson aongee kuna mzee na kuna mama, lakini Samson kwanza aje apeane maoni yake, tujaribu kufupisha mambo maana maneno mengi watu wameshapitia.

**Samson Losikinatum:** Maoni yangu ni kwamba, ninaona kwamba kuna hii nchi yetu ambaye wanataka, ku-create constituency, three constitutencies ama whatever, tungesema kama sisi wa Pokot kwamba hatutaki tuchanganywe na kabila nyingine. Kwamba wakati wana create a constituency ama wakati inatengenezwa location, tusichanganywe na sisi kabila nyingine, sisi kama inatakikana tufanye hivo sisi tupatiwe kama kabila ya Pokot.

Inginge tena ningesema kwa upande ya wale wazee wa kijiji wapatiwe mshahara kama wale Councillors. Wapatiwe pesa, mshahara pia kama wale Councillors, wapatiwe pesa kwa sababu hawo ni watu wa siasa kama wengine na wanafanya kazi kubwa, bali hawa...(inaudible)

Ningesema tena kuna (inaudible) nchi yetu hii Pokot kuna wale hawajiwezi hawana chakula, Serikali watenge chakula ambayo kama America wagawanyie watu kama hawana chakula wapatiwe (inaudible) kwa sababu kuna wale hawajiwezi, lazima Serikali ya Kenya wawalishe hawa.

Education nimesema ingekuwa free kutoka Nursery kama vile wenzangu wamesema.

Tena ningesema wakati tutapata kama vile wenzangu wanasema kwamba tunataka District, District tupatiwe kama kabila yetu ya Pokot na wakati tutapata district hii district tupatiwe Kortini yetu kwa area yetu, tuwe tusiende pahali kwa sababu mambo yetu ya Pokot (inaudible). Nafikiria ni hayo tu.

**Leiro:** Asante sana Bwana Samson. Kwa hivyo tumpate Councillor Musa Amoko

**Cllr. Musa Amoko:** Ningetaka kuongea kuhusu mambo yakurithi wanawake, hii mambo yakurithi wanawake wa Pokot wanakuwanga na wanawake karibu zaidi ya tano, na wakati huu hawo wanawake wale mlango yao, au kabila yao, huyu mtu unajua mtu ambaye anakuwa na wanawake tano kurudi na chini na wakati huo wale wandugu zake wanakuchua hawa wanawake kwa sababu ya watoto na ngombe, ningetaka hiyo kitu ipotezwe kabisa wa Pokot na hao watoto walishwe na sheria pamoja na wale watu wao pengine wamebaki wagawe kwa jamii hawa watoto pamoja na mama yao yaani iwe boma ya huyu mtu akiwa vile ilikuwa na kuchunga wakiwa boma yao. Kuangalilia mali yao pamoja na maisha wao mpaka hao watoto wakue na tena hii mambo yakurithi hawa wanawake wengi huwezi ukajua mambo ya ukimwi kama hawa wanawake wote ni wasafi au namna gani, lakini pengine unakubali jambo fulani (inaudible) haiwezekani kwa sasa kwa hivyo hiyo mambo itupiliwe mbali na hawa watoto wachungwe na watu wao wakiwa pale wakae na mali yao katika boma yao mpaka wajiwezeshe katika maisha



yao.

Halafu ningetaka kurudia ya kwamba Ma-Councillors, au locations katika (inaudible) wachaguliwe Councillors katika location ya watu mia tano, na ikiwa division ziko location nne ama tano, Councillor moja achaguliwe kama Tangulbei ama headquarters awe ni Mayor kuliko kwenda Kabarnet au kwenda Marigat au kwenda (inaudible) ati anaenda kuwakilisha watu kwa mambo ya plot au mambo ingine ambaye iko na uhusiano, Councillor mwingine achaguliwe kama Mayor hapa, mwingine achaguliwe kama Chairman hapa halafu apate kuwakilisha watu (inaudible) kwa sababu watu (inaudible) hii njia yote hii tulieenda hakuna magari tunaenda kulala Marigat au tunaenda Kabarnet kwa mkutano na tukikuja huku (inaudible) tunakuta imeenda tunakuja karibu siku tano kufika hapa. Kwa hivyo Serikali wafanye mambo ikuwe karibu kwa wananchi.

Halafu hii mambo ya wanyama, wanyama wanasumbua watu sana, wakati shamba inaharibiwa na wanyama wa Pori, serikali inawapatia hawa watu wa KWS kuwa hawa ndiyo walinzi wa wanyama na hawa watu hawajali maisha ya binadamu. Wanajali maisha ya wanyama zaidi kwa sababu hawa ndiyo investment hawa wanyama kwa watalii, kwa hivyo hawa wanyama mashamba ya wananchi ikiliwa na wanyama ilipwe. Walipwe na Serikali au walipwe na hiyo (inaudible) hiyo mnyama imetoka. Na hiyo kitu imetusumbua zaidi. Kwa mambo kama hii.

Mambo ya Constitutency, WaPokot hawa watu wafugaji wote including Pokot wajumbe wao awakilishe watu elfu kwa sababu ya watu ambae wanatoka area ambaye ni hardship kabisa. Tuna (inaudible) mahali wanajali wale watu wa Nairobi, Nakuru, kama pale kuna watu wengi isiwe wale watu hawajajua ni wote pamoja na (inaudible) anangali hao lakini watu ambae hawana masomo kama area watu Pokot, wanasema tu wanaletea hawa watu (inaudible) kwa hivyo area kama wawe tatu kwa hivyo wale wasiwe na Pokot. Nafikiri kwa hayo yote ...

**Leiro:** Asante sana Bw. Amoko, mtu wa mwisho ambae ataongea wa mwisho ambaye anapeana ni huyu mama ambaye anaitwa Chepocheboss Mailuk karibu mama.

**Chepcheboss Mailuk:** Soro nyo wou wena Amoko, chii nyopo sruum kuungalan kuroy Chepocheboss Mailuk, karibu yoo.

**Translator:** Jina langu Chepcheboss Mailuk.

**Chepcheboss Mailuk:** Kureenanuun Chepocheboss Mailuk.

**Translator:** Jambo ningelitaka kuipeana kwa ma Commissioners leo;

**Chepcheboss Mailuk:** Kuugh nyo ko-omoraan omwochuuney piipo Commission,

**Translator:** Nazungumza juu ya tohara ya wasichana.

**Chepcheboss Mailuk:** Ongolo neenan ngala muutat nyopo tipiin

**Translator:** Wale wanatahirisha hawa wasichana mara nyingi wanamshika huyu mtoto hata kama baba hajaruhusu wanaenda kumtahirisha huyu mtoto.

**Chepcheboss Mailuk:** Piichini lee muutii tipiin, ompo kungaat, nomoy akwanee tipiin ompo nguvu hata kama meetoh chii nyole papo owesyo.

**Translator:** Ningetaka tufanye tuweke namna hii

**Chepcheboss Mailuk:** Ko-omochan keegh lee nyonii.

**Translator:** Tutatanyia nini huyu ambaye anatahirisha mtoto wa mtu kabla mwenyewe hajamruhusu ama mzazi wake hajamkubalia.

**Chepcheboss Mailuk:** Kiydonee chii nyona muutoy momboo chii ktooma kuucham yiyiiindenyii nyaa?

**Translator:** Kwa sababu anakataa maneno yako halafu yeye anaenda kushawishi anaonekana baadaye (inaudible).

**Chepcheboss Mailuk:** Ompo wolo toghoy ngalee kuu atolapai kunguun kutepinyii kungaat.

**Translator:** Nataka huyo mama ambaye anafanya hiyo kazi ashikwe.

**Chepcheboss Mailuk:** Mchiini kokonyoon nyolee mutiin lee nyonii kenaam.

**Translator:** Kwa sababu mambo kama hii ikifanyika hata kama hukuwa na nia ya kwenda huko, unashindwa mahali pa kwenda kwa sababu hakuna sheria ambaye imewekwa kwa huyu mtu.

**Chepcheboss Mailuk:** Ompowolo ato yighiisyoo ngala cho lenyee chete, polinyii loo iwetenyii imwochiini ng'oo ompo wolo

mominyee sheria nyoo riipoy ngala mutaata.

**Translator :** Kwa sababu leo ni wakati wakubadilisha Katiba uweke katiba mpya kwamba mtu kama huyo akifanya hiyo kosa lazima achukuliwe kwa sheria.

**Chepcheboss Mailuk:** Ompo wolo aswaneete nyo kuwoyokoy katiba, ksomeecha lo mchiini kechenchiii chii nyo muutiin nyo muutoy monuung' o piich ompo nguvu sheria nyo kwaan.

**Translator:** Kuna wale watoto ambayo wanapewa mimba.

**Chepcheboss Mailuk:** Miteni monuungo chay kikiwoos,

**Translator:** Mtoto anapewa mimba halafu mwenye anafanya hilo kosa akatae ama aruke aseme si yeye.

**Chepcheboss Mailuk:** Sukooy monuung mimba atolapay kuruup chichiini keeto mimba kutaagh ngalechaai.

**Translator:** Wakikubaliana wakae anambiwa lipa faini kulingana na hii makosa ulifanya.

**Chepcheboss Mailuk:** Ato chaam kumongiisyo tukul, kelenchuu okonuuno tukuu kiwosaat.

**Translator:** Mara nyingi mambo kama hiyo ikifanyika watu wanachukua hiyo mali wanaenda naye yule mtoto anawachwa hajaolewa na yule mtu anapatiwa sasa kuchunga huyo mtoto, hata huyo mtoto anakaa nyumbani, huko nyumbani anapata huyo mtoto na uzito inaongezeka, (inaudible) mwingine anafanyika (inaudible) kwa hivyo tunataka kuonelea huyo mtoto ama hiyo mali ichukuliwe apatiwe huyo mtoto ajichunge naye badala ichukuliwe.

**Chepcheboss Mailuk:** Ompo kuungat, nyoman atoyighiisyo ngalee chooni, cheengooy piich tikuu chay po kiiwosaat kudong monung nko chichino kacheng mondo, nyo mchiini kesuwaa loo kiitoni monuungiini tukuu chiini kapkana kiwosaat.

**Translator:** Kila mara tumesoma visa ambayo inajina ambayo (inaudible) kwa sababu wakati mwingine mtu anaoa bibi yake anaenda anaishi yule (inaudible) anaenda kutafuta kibarua anaenda (inaudible) sasa huyu mtu anaporudi anakuta yule bibi amechukuliwa na mwingine, amezaa mtoto anaishi sasa anakuja kuandikisha case anasema huyu mtu alichukua bibi yangu kwa hivyo anataka huyu mtu alipe hiyo fine sasa tutafanye kitu kama hii kwa sababu hii ni ajabu kwangu Commissioners.

**Chepcheboss Mailuk:** Kungat, ngeetoy chii kupuustoy katanyii akuuwoo kwiip korkaa angaa, atolapay kungeet korkonay kuyarataa kasiine chii ak-nyooru muroon nyo kachaam kwiip muronoo naai nko monuunge chii. Nguunoy chiichay po tagh kiip

kamanay kwiiipu kesii kungaat, akuloo korkenyaan nyara angwa nyiino kipuusto nyindee.

**Translator:** Kwa hivyo Katiba ya leo izingatie maneno kama haya kwa sababu imekuwa shida nyingi sana aina hii na huyu mtu kwa sababu hakuna njia nyingine ambayo (inaudible) anasema kweli ni huyu mtu halafu mambo mengi, yule mtu analipwa hiyo fine, kwa sababu alifanya hivi anaenda mwaka kumi au mwingine mwaka ishirini anakuta ule mtu ame (inaudible) Kwa hivyo hii Katiba ya leo izingatie maneno kama hayo. (inaudible) ya kwamba huyo mtu kama alienda hiyo miaka yote na kumbe bibi amepata watoto wawili au watatu aseme asante halafu aende amwambie yule mtu angalau unirudishie bibi badala ya (inaudible) Kwa hivyo Katiba ya leo iangalie hiyo maneno.

**Chepcheboss Mailuk:** Kikluuku tongoonchiin nyoman wechara, nyo mchiini katiba nuu reel kuroos ngalee cheete nyoman ompowolo nguunoy chiichay kwaam kaa chii angwanyiino kiipustoo korkoo niini ompo konyiis cho chang nyoman lenye taamaan, wetoy kungaat lee nyayee atolapay kunguun kikeep kokonai, kchoogh kesii kungaat.

**Translator:** Mzee saa zile watoto kama wako (inaudible) mzee anatakiwa wa miaka kumi na huyu mzee ni wa sixty years, sasa kwa sababu yeye anauwezo wa mali, yuke mzee ndiyo anapewa mtoto. Sasa mawazo ya yule mzee na yule mtoto hawakutani sasa hiyo inaleta maneno nyingi. Naona msichana huyo anaamua kunywa sumu anakufa ama anatoroka (inaudible).

**Chepcheboss Mailuk:** Kiitoo anga kuu ngala monuung cho kiyiilchini anda kichuut- chiini pooy cho gheechon lenyee konyiis 60 nko cheptoo nyo munuung. Ompowolo mongorion chichay, keyiilchuu paat monuung nyoo munuung atolapay kwaam monuung sumu ompo wolo meemukiisyoo nyee mongoot nko chii chooni.

**Translator:** Tunataka Katiba ya sasa isiruhusa tusiwalazimisha watoto wetu kuolewa na wazee.

**ChepCheboss Mailuk:** Kmookeecha katibanu poo yee mee-lasimishan monuungee chaa.

**Translator:** Na kama moja amepatiwa mimba kama kutakuwa na fine, ile fine sasa watu wasikule, apatiwe ile mzee baba ya mtoto, achunge wale watoto.

**Chepcheboss Mailuk:** Ato kiiwoos monuung, akmiiteni fain, keeto kuukotoo monuung kuriipo monuung, momchiini nyee kwaam nyiinde.

**Translator:** Kama kuna mtu anapatia mtoto wa mtu mimba na akiwa anafanya kazi na ana pesa yake ikatwe imlishe yule mtoto mdogo.

**Com. Hassan:** Nataka kumuliza swali moja, anasema kama msichana akiwekwa mimba, kuna fine inalipwa ya mbuzi na ngombe, kama hiyo mbuzi hapewi huyo msichana, anapewa nani?

**Chepchoboss Mailuk:** Chengoy yiyii koo cheptoo maliichay poo kiwoosat.

**Translator:** Wakati wanachukua hiyo mali, ni wazazi wake, tuseme ni family yake.

**Com. Hassan:** Kwa nini hawa chukua kwani hawa ndiyo wamewekwa mimba? Kwa nini hawa wanachukua?

**Translator:** Ompo nee nya takcheengooy, akwanee soo choo kakiiwoos?

**Chepchoboss Mailuk:** Kiimiteni ngalee chetee lee nyooni kuupo koony nyo mchiini akurokonee katibanuu reel kuwayaak ngale chooni.

**Translator:** Hii maneno hajui kwa sababu ile ya constitution ya wazee ile haijaandikwa ilikuwa inaruhusu hivyo, lakini kwa sababu leo tunabadilisha Katiba, kwa hivyo sasa hiyo Katiba ihakikishe ili (inaudible)

**Com. Baraza:** Okay mama Chepchoboss, umesema kwamba watu wana tahirisha wasichana sheria imekuja bunge sijui kama nyinyi mumesikia, iko sheria imepitishwa bunge inaitwa sheria ya watoto, na mtu hata kama wewe kama ni mama au baba wa huyo msichana ukichukua msichana ambaye hajafikisha miaka kumi na nane umtahirishe hiyo ni hatia, wewe mwenyewe kama mzazi utashikwa na mtu ambaye atachukua mtoto amtahirishe kwa lazima huyo pia atashikwa, umelewa? Sheria imepitishwa kuharibu, umelewa sheria imepitishwa umelewa? Kupasha tohara msichana unashikwa unaletwa kortini hata unaweza kunyongwa. Na ukifika miaka kumi na nane kama ni msichana mwenyewe hataki hakuna mtu atamshika ati amtahirishe, mwenyewe labda apende, aseme wacha nitahirishwe, lakini yule ambaye hajafikisha miaka kumi na nane iko D.O. hapa, iko sheria imepitishwa bungeni. Na kama mtu akichukuwa mtoto wako atahirishe enda kortini au kuja Nairobi uwaulize hawa wa mama wanaongea hii maneno yakutahirisha, umelewa?

**Translator:** (inaudible) Wakati anaoza msichana

**Chepchoboss Mailuk:** Otinii kakiiwoos cheptoo,

**Translator:** Wanaitagwa huyo mama ni bure

**Chepchoboss Mailuk:** Ku-kuuroy yoo niini kulee.

**Translator:** Hata kama umekataa, ulikuwa na niya yakumkataa huyo mtu, kama tu mtu anaomba msichana yako, hata kama ukisema hapana bora mzee amekubali, kwa hivyo sauti ya mama hakuna mtu anasikia.

**Chepcheboss Mailuk:** Lendoy, wechara, kleenyeechaa kulee piich chole yootun, ompowolo hata, keetagh keyiip cheptoonguuu akik-chaam chii nyolee papoo, momiinyee kuugh nyo iyiigheenyii.

**Translator:** (inaudible) mtot ni kila mtu siyo wa baba peke yake, kama (inaudible) basi mambo inakuwa namna hiyo, asante sana.

**Leiro:** Bwana Commissioner nafikiri wale watu wamejiandikisha, wale watu ambayo bado hawajawasilisha maoni yao, isipokuwa kuna moja amesema angeuliza kama anapewa nafasi, lakini zaidi kama vile.....

**Com. Hassan:** Kuna mtu yeyote ambaye ataongea bado ambaye anataka kuongea? Yes Officer,

**James Lukuyat:** Kwa majina ninaitwa James Lukuyat, Ningeongea kuhusu upande hii ya wa mama na wasichana, wa mama wakismama hapa nakutetea siku ya (inaudible) lakini kuna kwa maoni yangu naona hawajaandika vizuri (inudible) sehemu hii ya Pokot tumepata shida kwa upande ya wasichana kuna watu wachache wamejaribu kutuma wasichana shule, na hawa tumechukua kama mfano, wamekabiliana na ile yakuwekwa mimba na inachukuliwa kama mchezo tu, lakini ningeshukuru kulingana na vile Commissioner wametuambia kwamba kuna sheria siyo sheria ya wale kabila zingine inasimamia hata sisi kama jamii ya waPokot, kwa hivyo ningewaomba hawa watu kwamba, mtumie sheria sababu watu watu wanawacha hata shule ya upili kutokana na shida yakutiwa mimba na ukijaribu kuingilia kama officer hawaisaidii, mzazi mwenyewe haelewi kama mtoto wake amepata shida, shida imengia kwa hivyo nafikiri tunge zingatia kabisa tutanufaika kabisa kwa hii sheria (inaudible)

Jambo jingine tumekuwa na shida na mambo ya uchawi, hii mambo ya uchawi kwa Katiba ya hapo awali kuna pahali ilikuwako ama hapana, kama ilikuwa hakuna, na hii Katiba tunarekebisha tuweke wapi uchawi? Sababu nilisikia mara kwa mara wa upande ya Kisii nasikia mtu amewekwa tairi amechomwa na kuchoma binaadamu namna kama hio haifai. Maoni yangu nineiona tu hii Katiba tunayetafuta tufuate tuweke wapi hii uchawi ambapo tusikumbane na hii mambo yakua binadamu nakuchoma kama si kitu ya maana. Ni hayo tu.

**Leiro:** Asante sana bwana James.

**Patrick Litikit:** Asante sana Bw. Commissioner tangu awali nilikuwa napokea kama watu wanaongea lakini ningetaka kuchukua fursa hii niseme yangu moja,

**Com. Hassan:** Sema jina lako

**Patrick Litikit:** Jina langu naitwa Patrick Litikit. Maoni yangu ambayo ninapatia hii Commission kwa sheria ya sasa ni kuhusu mambo ya Pastoralists. Nilikuwa nataka hii commission ya leo ambaye imepitisha sheria ambayo inatungwa siku hizi, isisitize kwamba katika zile districts ambaye tuko naye, nafikiri tuko nayo tangu kama 27 itunge a Ministry called Ministry of Pastoralists. The Constitution should look into a way of creating Pastoralists Ministry and the reason is kila Ministry pastoralism hawangaliwi mambo yao vizuri kwa hivyo hii district ambaye itakuwa created inataka hiyo district iwe headed by a Pastoralist Permanent Secretary na pia hata Minister should come from a Pastoralist Community kwa sababu mara nyingi watu ambaye wameshindwa itakuwa ni Pastoralists kwa hizi Ministry zingine. Naona ya kwamba (inaudible) from non pastoralism affairs while huyo mtu haelewi yeyote kuhusu mambo ya ng'ombe, huyu ni mtu ambaye tangu utotoni wake hajawahi kuona ng'ombe pia hajui how well animal na hajui shida za pastoralists, kwa hivyo tukiwa na Ministry ambaye ni ya area ya Pastoralists hivi ambayo (inaudible) pastoralism wataweza kusaidika kwa sababu mara nyingi wabunge wakisema mimi natoka pastoralist community unaonekana kama hujui kitu hata ukiwa na degree ambaye hata umeenda somea chuo kikuu ambayo ni recognized. Watu ambaye (inaudible) lakini ukisema mambo ambayo ina husu mambo ya (inaudible) lakini hii ni kwa sababu udhaniwe tuu, huyu mtu anatoka jua kali hajui kitu chochote, kwa hivyo ninafurahi kuona ya kwamba hata hii Commission kuna watu ambayo ni Pastoralists ambaye wanachukua maoni kwa hivyo ni mchango wenu pia kama Commissioners although ya kwamba tunachangia to create that Ministry called Ministry of Pastoralists so that Pastoralists affairs can be looked into. Asante..

**Leiro:** Asante sana Bw. Patrick, Tuko hapa na D.O. aje atufungie na apeana maoni yake kwa hii Constitution ya leo. Kwa hivyo karibu Bw. D.O.

**District Officer:** Asante sana Chairman wa Kamati hii ya kikao hichi chetu cha leo, mimi sitatoa maoni kwa leo, kama ni maoni yangu nitaandika nyaraka na nitawapatia Commission, yangu pengine nikutoa kilma cha shukrani. Ningependa kutoa kilma cha shukrani kwanza kwa Ma-Makamishna ambao wamejikokota kutoka huko walikotoka mpaka kufika Tangelbei, ni mbali sana na najua walichoka sana lakini wametimiza na wamekuwa nasi na wamekuwa wavumilivu mpaka wakati huu wote mpaka kufikia saa hii.

Pili ningependa kuwashukuru tena hao hao ma-Kamishna kwa kuchagua Tangelbei kama kituo cha kuchukua maoni kwa wananchi, si kila mahali ambapo Kamishnas munaweza kuwapata kama hivi, kwa hivyo nimesema ni shukrani kwani wa Pokot wakutoka Tangelbei wamepata fursa yakuweza kijieleza yale wangetaka katika Katiba yao. Unaona kwamba Katiba ni kitu muhimu, Katiba itakuwezesha wewe, itakusaidia wewe kama mtu ambaye unaishi wakati huu, itamsaidia mtoto wako, itamsaidia mjukuu wako, itamsaidia kitukuu wako, itamusaidia kilembwe, itamsaidia kilembwe keti mpaka (inaudible) kwa hivyo yale ambayo mnafanya hapa msione kama ni mambo ya kipuzi ni mambo ambayo ni muhimu kabisa, na ni mambo ambayo yatamtumikia kila mwananchi hapa Kenya.

Kwa hivyo tena tatu nawashukuru nyinyi wenyewe wananchi wa Tangulbei kwa kujitokeza, tumeona hapa mambo mengi ambayo yamezungumzwa, tumeona hata Serikali za kina baba sasa ndiyo karibu kupinduliwa kwani kumetokea kina mama wanasema kuwa mambo ya mahari hamuwangalii, mukipata mahari ni yenu na wandugu zenu, kwa hiyo nafikiri munaona vile ambavyo changa moto zilitoka na tulipata mawaidha mengi kutoka hapa na pale, hiyo ni shukrani na tungependa kama kutakuwa na vikao vingine zaidi basi muweze kujitolea. Namuambia kwamba kutoa maoni hapa siyo mwisho, hapa bado siyo mwisho, mpaka sasa una fursa yakuweza kuandika waraka wowote na upeleke kwa Commissioners ambao watauchukua na pia utaangaliwa. Kwa hivyo usiseme kwamba nikikosa hapa leo sina fursa tena, fursa bado iko mpaka siku watakao funga kazi yao, lakini bado hawajafunga kwa hivyo yoyote ambayo hakutosheka na anaona kuna kitu ambayo amesahau mahali basi kipengele hicho aweze kukiandika akipeleka kwa wanao husika na zitachukuliwa. Kwa hayo machache na hayo nafikiri mumegusiwa kuhusu mambo ya tohara ama kupeleka watoto jangwani, mumeambiwa pia kinaga ubaga kwamba tatizo hilo lilikabiliwa na Serikali na sasa kuna sheria, na sheria hiyo ni kali ni wajibu wa msichana wako, ajitambulie mwenyewe akifika umri wa miaka kumi na minane aseme nataka kutahiriwa na atahiriwe na pia hata Katiba wakati huo atahiriwe kwa ile njia inayofaa, ile ambayo haiwezi kumpatia magonjwa kama haya munayo sikia ya ukinwi na kadhalika; ataweza kwenda kutahiriwa hata hospitali, lakini uamuzi ni wake mwenyewe akifika miaka kumi na minane. Usimulazimishe, na wengine nasikia wameanza kutayarisha mangoma ngoma na kadhalika yakupeleka watoto kiandoni, mujue sheria iko na munaweza kuchukuliwa hatua wakati wowote kwa hayo mengi na hayo machache natoa shukrani zangu tena kwa Ma-Commissioners, nawaombea kila na heri popote wanapo enda kufika salama waweze kupata maoni, tukitoka hapa tuweze kupata katiba ambaye ingeweza kusaidia kila mwananchi mkubwa kwa mdogo. Asanteni.

**Leiro:** Asante sana bwana District Officer, nitarudisha sasa kwa upande wa Commissioners kama kuna neno ambayo wanataka kuongeza ama kuna kitu kusema kabla hatujafunga kikao hiki cha leo. Karibu Bw. Commissioner.

**Com. Hassan:** Asante sana Bw. Chairman, tunawashukuru watu wa Tangulbei kwa yale maoni mumetoa kwa kweli tumepata maoni nyingi nzuri, na tukimaliza kuchukua maoni Baringo Constituency, tutaenda Western Province, tukimaliza tunatarajia kutengeneza ripoti ya National Report na ile ya Constituency Report yaani kila constituency tunatengeza ripoti yao na baada ya mwezi moja tunatarajia kurudisha kwa kile constituency kwa hivyo itarudi hapa tena Tangulbei na Kollowa na pahali pengine ambae tutaenda kuchukua maoni, ripoti itarudi tena ndiyo muone watu wa Tangulbei ile ripoti ile tunaandika kwa kweli mulitoa maoni yenu, mulizingatia na kama kuna maoni ingine ambaye mulichangia hapo pia mutatueleza lakini hiyo ripoti itakuja tena hapa ndiyo muone kwa kweli ni yale maoni yenu ambaye mumetuambia ya kwamba leo imezingatiwa. Kwa hivyo hiyo ripoti ikikuja tunataka watu wa Tangulbei musome, muangalie ya kwamba maneno ambayo mulikuwa mumeyasema yamezingatiwa. Na vile D.O. amesema tunachukua maoni mpaka tarehe kumi na tano mwezi wa saba, kwa hivyo kama unafikiri ungependa kuna kitu tutengeneze kwa ile ripoti ingine, mukuwe tu na hiyo fursa yakutengeneza maoni yako mpaka tarehe kumi na tano mwezi wa saba. Unaweza kumpatia kuonyesha ambaye pia (inaudible). Kwa haya machache ningependa kuwashukuru Ma-committee members na kuwapongeza kwa ile kazi ile mumetufanyia hapa leo na naona tufunge hii kikao na maombi.



**Leiro:** Kwa hivyo kabla hatuja funga tungependa kuwashukuru wote ambao mumeshiriki, mkatoa maoni yenu najua ulikuwa na kazi nyingi lakini uliona kikao hiki ni kama kikao cha maana ndiposa umekuja kuwa na patience kutoa maoni yenu. Ni madhumuni yangu ya kwamba yale yote mulizungumza itabidilisha maisha yetu siku za usoni kwa hivyo maoni haya haikuwa tu kupena, lakini ilikuwa inapeana iende isaidie kwa vizazi vijavyo, kwa hivyo nashukuru viongozi wote ambao wamehudhuria na mimi yale yote mulileta ni maoni ya wote watu, watu wa hapa wote hawawezi kuingia katika jumba hili lakini waliwa mandate wale wamekuja kupresent their views and I know from tomorrow you will hear what you talked and they will be very happy so I thank the Commissioners for this historic visits.

I have never been happier like this since independence we have not had a forum of this type where our people give their views in such a manner. I think this one was meant to say, it is not like those ones you normally hear from the paper, oh it is like this or like that but today you have seen for yourself and you have heard from the horse's mouth. Kwa hivyo hayo maoni yamepeanwa ni maoni ya maana na ni maoni ya kweli kwa hivyo nawashukuru sana and I know tomorrow mutakuwa huko Nginya, kesho kutwa tutakuwa Kollowa kwa hivyo tuakuwa pamoja na mengi mtasikia kwa hivyo tuchukua Pastor moja atuombee. Kuna Pastor Mailuk unaweza kutufungia kwa maombi.

**Pastor Mailuk:** Natuombee. Baba wetu aliye mbinguni Baba, Yesu Kristo, tunakushuru siku ya leo kwa nafasi hii ambayo tumekaa hapa kwa huo muda yote mpaka tukafikia mwisho. Asante Mungu wetu kwa maana umetuwezesha kwa yale yote ambayo tumezungumza. Tunaona ya kwamba yale yote ambayo tumezungumza ni mambo ambayo yanatuongoza katika nchi hii na tunashukuru Mungu kwa maana tumemaliza saa hizi. Lakini yale yote ambaye tumeweka katika mavitabu Mungu aweze kutusaidia katika kuishi katika hii dunia. Asante Mungu kwa maana tunajua ya kwamba mambo yote inatoka kwako na Mungu wetu utuongoze katika yale maandiko yote ambayo tumeandika ili kile kitu ambaye tumeandika kiwe kitu ambaye kitatusaidia kuishi katika hii dunia. Asante Mungu wetu kwa wakati kama huu, huu ni wakati mzuri ambaye tunafurahia maana tumesikia (inaudible) kwa hivyo Mungu wakati tunapotoka sasa uwe unatoka nasi, hata wale watu wetu ambaye walitoka Nairobi leo wakienda wakirudi Mungu uwaongoze katika barabarani na uwalinde katika gari kila mahali na uwabiriki hata mkutano wao. Asante Mungu wetu kwa maana tunajua kwamba hakuna mwingine mlezi bora kuliko wewe, Yesu Kristo ambayo mwongozi wetu wa wote. Kwa hivyo utubarikie na utuongoze naomba katika Jina la Yesu Kristo muongozi wetu. Amen

\*\*\*\*\*